17. Bila ya kujali masharti ya sheria nyingine yoyote, hakutachukuliwa hatua yoyote au shauri lolote litakalofunguliwa dhidi ya mjumbe yeyote wa Baraza, Kamati zake, afisa au mwajiriwa yeyote kutokana na kitendo chochote au jambo alilofanya au kutaka kufanya kwa nia njema wakati wa utekelezaji wa mamlaka aliyopewa chini ya Sheria hii.

**SEHEMU YATATU
USAJILI NA UTOAJI WA LESENI KWA MADAKTARI NA
MADAKTARI WA MENO**

Aina za usajili

18.-(1) Aina za usajili wa madaktari, madaktari wa meno chini ya Sheria hii zitakuwa kama ifuatavyo:

- (a) usajili awali;
- (b) usajili wa muda;
- (c) usajili wa kudumu; na

(d) usajili wa kipindi maalum.

Utunzaji wa Rejista

19.-(1) Kwa madhumuni ya kifungu cha 18, Baraza litaanzisha na kutunza Rejista ya madaktari na madaktari wa meno wenye sifa chini ya Sheria hii.

(2) Daftari la usajili lililoanzishwa chini ya kifungu hiki litajumuisha taarifa za usajili na taarifa nyingine zozote kama itakavyoainishwa na Baraza.

Sifa za usajili

20.-(1) Mtu hatakuwa na sifa za kusajiliwa chini ya Sheria hii isipokuwa pale mtu huyo atakapoliridhisha Baraza kuwa:

(a) endapo ni daktari, au daktari wa meno, awe na shahada ya kwanza katika fani ya tiba au tiba ya meno kutoka chuo kinachotambuliwa;

(b) endapo ni mtaalam wa saikolojia ya utabibu au mtaalam wa mazoezi ya viungo, awe na Shahada ya kwanza ya saikolojia ya utabibu au mazoezi ya viungo kutoka chuo kinachotambuliwa; na

(c) taaluma na utendaji wake kwa jumla unampa sifa ya kusajiliwa kama daktari au daktari wa meno kama itakavyohitajika.

(2) Waziri, baada ya kushauriana na Baraza, atatengeneza kanuni zitakazoainisha sifa za nyongeza au mahitaji ya usajili kama itakavyoona inafaa.

Utaratibu wa usajili

21.-(1) Mtu anayetarajia kupata usajili chini ya Sehemu hii, atawasilisha maombi kwa Msajili kwa kutumia fomu maalum.

(2) Maombi chini ya kifungu kidogo cha (1) yataambatana na:

(a) nakala iliyothibitishwa au nakala ya vyeti vya taaluma za mwombaji;

(b) ada ya maombi kama ilivyoainishwa katika kanuni.

(3) Msajili baada ya kupokea maombi, atawasilisha maombi hayo pamoja na mapendekezo yake kwa Baraza kwa ajili ya kufikiriwa na uamuzi.

(4) Baraza baada kutafakari maombi ya usajili, linaweza-

(a) kuidhinisha maombi na kumwagiza Msajili kumsajili mwombaji;

(b) kukataa maombi na kumwagiza Msajili kumtaarifu mwombaji juu ya sababu za uamuzi wa Baraza .

Cheti cha usajili

22.-(1) Baada ya kumsajili mwombaji chini ya Sheria hii, Msajili atatoa cheti cha usajili mara moja kwa kila daktari, au daktari wa meno aliyesajiliwa baada ya kulipa ada.

(2) Cheti cha usajili kitakuwa na:

(a) jina kamili na anwani ya mwombaji;

(b) sifa za kitaaluma na cheo cha mwombaji; na

(c) vigezo na masharti kuhusu cheti ambacho kimetolewa.

- Matumizi ya jina **23.** Mtu aliyesajiliwa chini ya sheria hii kama daktari au daktari wa meno atastahili:
- (a) kutumia jina na cheo kuhusu daktari au daktari wa meno kulingana na cheo kilichopo katika cheti cha usajili na hataruhusiwa kutumia cheo kingine chochote zaidi ya kilichopo katika cheti cha usajili;
 - (b) kutoa huduma kama daktari au daktari wa meno na kudai, kushtaki au kurudishiwa gharama kutoka mahakama yoyote ya huduma za kitaalam, msaada, ushauri au udhurio lolote la kwenda mahakamani.
- Mafunzo kwa vitendo **24.**-(1) Mtu yeyote anayekusudia kufanya mafunzo kwa vitendo, atatuma maombi kwenye Baraza ndani ya miezi mitatu baada ya kuhitimu shahada ya kwanza, kwa ajili ya kupewa usajili wa awali.
- (2) Dakatari au daktari wa meno aliye na usajili wa awali, baada ya kusajiliwa, atatakiwa kuripoti kwenye kituo cha mafunzo kwa madhumuni ya kufanya mafunzo kwa vitendo, na iwapo atashindwa kuripoti kwenye mafunzo usajili wake wa awali unaweza kufutwa.
- Usajili wa awali **25.**-(1) Daktari au daktari wa meno mwenye usajili wa awali hataruhusiwa kufanya mafunzo kwa vitendo hadi pale Baraza litakapompatia usajili wa awali.
- (2) Utaratibu na matakwa ya usajili wa awali yatakuwa kama yatakavyoainishwa kwenye kanuni.
- (3) Mtu atakayepata usajili wa awali, baada ya kulipa ada iliyoainishwa, atapewa cheti cha usajili wa awali.
- (4) Daktari au daktari wa meno mwenye usajili wa awali atachukuliwa kuwa amesajiliwa ili kumwezesha kufanya kazi chini ya uangalizi wa daktari au daktari wa meno mwandamizi aliyesajiliwa.
- Usajili wa muda **26.**-(1) Daktari au mtaalam wa meno ambaye atakuwa amehitimu mafunzo kwa vitendo atapewa usajili wa muda baada ya kutuma maombi kwenye Baraza.
- (2) Kipindi cha usajili wa muda kilichoorejewa chini ya kifungu kidogo cha (1), kitakuwa miaka miwili ambapo daktari au daktari wa meno atafanya kazi chini ya uangalizi wa kiasi.
- Usajili wa kudumu kama daktari na daktari wameno **27.** -(1) Mtu ambaye, amehitimu mafunzo kwa vitendo na kufanya kazi kama daktari au daktari wa meno kwa muda wa miaka miwili chini ya uangalizi wa kiasi, baada ya kuwasilisha maombi kwenye Baraza, atakuwa na haki ya kupatiwa usajili wa kudumu kama mtaalam daktari au daktari wa meno.
- (2) Maombi ya usajili wa kudumu chini ya kifungu hiki yataambatana na:
- (a) nakala ya cheti cha usajili wa awali na wa muda; na

(b) taarifa nyingine zozote kama zitakazohitajika kwa madhumni hayo.

Usajili wa wageni

28.-(1) Mgeni anayekusudia kufanya kazi kama daktari au daktari wa meno chini ya Sheria hii, atawasilisha maombi kwenye Baraza pamoja na nakala za vyeti vya taaluma na taarifa nyingine zozote kama zitakavyoainishwa kwenye kanuni.

(2) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), mgeni atastahili kupata usajili wa kipindi maalum.

(3) Muda wa usajili wa kipindi maalum utakuwa kama utakavyoainishwa kwenye Kanuni.

Usajili wa watu waliohitimu nje ya Tanzania

29.-(1) Mtu aliyehitimu nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama daktari au daktari wa meno atafanyiwa tathminiwa na Baraza juu ya elimu na ujuzi kabla ya kufikiriwa kupewa usajili anaoomba.

(2) Utaratibu wa tathmini uliorejewa chini ya kifungu kidogo cha (1), utakuwa kama utakavyoainishwa kwenye kanuni.

Kufuta au kusitisha cheti

30. Endapo mmiliki wa cheti atashindwa kuzingatia masharti ya yaliyowekwa kwenye cheti cha usajili kama inavyotakiwa, Baraza linaweza kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 31, kufuta au kusitisha cheti cha usajili alichopewa chini ya Sheria hii.

Utaratibu wa kusitisha cheti cha usajili

31.-(1) Endapo dakatari au daktari wa meno amekiuka vigezo na masharti ya usajili wake, Msajili baada ya kupokea maelekezo ya Baraza, atampatia daktari au daktari wa meno atampatia taarifa maandishi ikielezea aina ya ukiukwaji.

(2) Baada ya kupokea taarifa chini ya kifungu kidogo cha (1) daktari au daktari wa meno kama itakavyokuwa, atawasilisha utetezi wake kwa maandishi kwa Msajili kuhusu kurekebisha ukiukwaji huo.

(3) Daktari au daktari wa meno atakayeshindwa kurekebisha ukiukwaji huo ndani ya muda ulioainishwa katika taarifa au akushindwa kuwasilisha utetezi wa kuridhisha kwa Msajili, Msajili atalishauri Baraza kufuta au kusitisha cheti cha usajili.

(4) Endapo Baraza litaridhika na ushauri chini ya kifungu kidogo cha (3), litamwagiza Msajili kufuta au kusitisha cheti cha usajili.

Leseni ya kutoa huduma

32.-(1) Mtu ambaye ni daktari au daktari wa meno na anataka kutoa huduma chini ya Sheria hii, atatuma maombi kwenye Baraza kwa ajili ya leseni ya kutoa huduma.

(2) Maombi ya leseni ya kutoa huduma yaliyorejewa chini ya kifungu kidogo cha (1) yataambatana na:

(a) cheti cha usajili;

(b) ada ya usajili; na

(c) nyaraka nyingine zozote kama Baraza litakavyoona inafaa.

(3) kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2), Baraza linaweza:

- (a) kuidhinisha maombi na kumwagiza Msajili kutoa leseni ya kutoa huduma kwa mwombaji; au
- (b) kukataa maombi na kumwagiza Msajili kumfahamisha mwombaji juu ya sababu za uamuzi wa Baraza.

Kuhuisha leseni ya kutoa huduma

33.-(1) Leseni ya kutoa huduma iliyotolewa chini ya kifungu cha 32 itahuhuishwa baada ya kulipa ada iliyoainishwa.

(2) Leseni ya kutoa huduma, haitahuishwa mpaka pale mwombaji atakapothibitisha kuwa amefanya masomo endelevi ya taaluma ya udaktari kama itakavyoainishwa katika kanuni.

(3) Taratibu za kuhuisha leseni ya kutoa huduma itakuwa kama ilivyoainishwa katika kanuni.

SEHEMU YA NNE

UORODHESHWAJI, UANDIKISHWAJI NA UTOAJI WA LESENI KWA WATAALAM WA AFYA SHIRIKISHI

Masharti ya kuorodheshwa na kuandikishwa

34. Mtu anayetaka kutoa huduma kama mtaalam wa afya shirikishi kabla ya kutoa huduma, atapaswa kuorodheshwa au kuandikishwa na Baraza.

Sifa za kuandikishwa na kuorodheshwa

35.-(1) Mtu-

- (a) ataandikishwa na Baraza kutoa huduma kama mtaalam wa afya shirikishi iwapo mtu huyo ana stahhada ya juu au stahhada kutoka katika chuo kinachotambulika; au
- (b) ataorodheshwa na Baraza kutoa huduma kama mtaalam wa afya shirikishi iwapo mtu huyo ametunukiwa cheti kutoka chuo kinachotambuliwa na Baraza.

(2) Waziri anaweza, kwa kuzingatia mapendekezo ya Baraza na kupitia Tangazo la Serikali, kuainisha vyeti vingine au sifa zitakazomwezesha mwanataaluma kuandikishwa au kuorodheshwa chini ya Sheria hii.

Utaratibu wa kuandikishwa au kuorodheshwa

36.-(1) Mtu ambaye anakusudia kuandikishwa au kuorodheshwa kama mtaalam wa afya shirikishi, atawasilisha maombi kwa kutumia fomu maalum kwa Msajili.

(2) Fomu ya maombi chini ya kifungu kidogo cha (1) kitakuwa na taarifa kama zitakavyoamuliwa na Baraza na itaambatana na:

- (a) nakala ya iliyothibitishwa au vyeti vya muombaji vya taaluma; na
- (b) ada ya uandikishwaji au uorodheshwaji kama itakavyoainishwa na Baraza.

Utoaji wa cheti cha kuandikishwa au kuorodheshwa

37.-(1) Kwa kuzingatia maelekezo ya Baraza, na baada ya kulipa ada iliyoainishwa, Msajili atatoa cheti cha kuandikishwa au kuorodheshwa kwa kila mtaalam wa Afya shirikishi kama itakavyoelekezwa.

(2) Cheti kitakachotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1), kitasainiwa na Mwenyekiti na Msajili, na pale kitakapohitajika kutolewa kitapokelewa kama ushahidi wa kuandikishwa au kuorodheshwa chini ya Sheria hii.

(3) Katika kutoa cheti cha kuandikishwa au kuorodheshwa kwa mtaalam wa afya shirikishi chini ya Sheria hii, Baraza litaweka masharti ya jumla au maalum yatakayozingatiwa na mwenye cheti.

(4) Endapo maombi ya kuandikishwa au kuorodheshwa hayakuridhiwa, Baraza litamwagiza Msajili kumtaarifu mwombaji kwa maamdishi kuhusu maamuzi ya Baraza na kutoa sababu.

Leseni ya kwa mtaalam wa afya shirikishi

38.-(1) Mtu aliyeandikishwa au kuorodheshwa chini ya Sheria hii na anataka kutoa huduma kama mtaalam wa afya shirikishi atatuma maombi kwenye Baraza kwa ajili ya kupata leseni.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), Baraza linaweza-

(a) kuidhinisha maombi na kumwagiza Msajili kutoa leseni ya kutoa huduma kwa mwombaji; au

(b) kukataa maombi na kumwagiza Msajili kumtaarifu mwombaji kuhusu sababu za uamuzi wa Baraza.

Kuhuishwa kwa leseni ya mtaalam wa afya shirikishi

39.-(1) Leseni ya kutoa huduma iliyotolewa chini ya kifungu cha 38, itapaswa kuhuishwa, baada ya kulipa ada iliyoainishwa.

(2) Utaratibu wa kuhuisha leseni ulioainishwa chini ya kifungu cha 33, utatumika sambamba na uhuishaji kama ulivyo chini ya kifungu hiki.

Msajili anaweza kuitisha taarifa za ziada

40. Msajili anaweza, ama yeye binafsi au kwa maelekezo ya Baraza, kumuomba mtoa huduma yeyote kuwasilisha kwake taarifa muhimu kuhusu sifa alizonazo.

Kufuta au kusitisha kwa muda cheti cha kuandikishwa au kuorodheshwa

41.-(1) Endapo mmiliki wa cheti cha kuandikishwa au kuorodheshwa atashindwa kuzingatia masharti yaliyowekwa kama inayotakiwa, Baraza linaweza kufuta au kusitisha kwa muda cheti cha kuandikishwa au kuorodheshwa kilichotolewa chini ya Sheria hii.

(2) Masharti ya kifungu cha 31 yatatumika kuhusu utaratibu wa kufuta au kusitisha kwa muda cheti cha kuandikishwa au kuorodheshwa chini kifungu hiki.

Kuandikishwa au kuorodheshwa kwa wageni

42.-(1) Mgeni yetote mwenye stahhada ya juu, stahhada au cheti na ambaye anataka kuorodheshwa au kuandikishwa kama mtaalam wa afya shirikishi kwa muda maalum, ataorodheshwa au kuandikishwa kwa muda.

(2) Utaratibu wa kuorodheshwa au kuandikishwa kama mgeni chini ya kifungu hiki, utainishwa katika kanuni.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YANAYOHUSU NIDHAMU

Usimamizi wa
utaratibu wa
malalamiko

43.-(1) Endapo daktari, daktari meno au mtaalam wa afya shirikishi atatuhumiwa kutokuwa na uwezo au sifa ya kutoa huduma, tuhuma hiyo itawasilishwa kwa Msajili ambaye naye ataiwasilisha mbele ya Baraza.

(2) Daktari, daktari wa meno au mtaalam wa afya shirikishi atachukuliwa kuwa hana sifa za kutoa huduma chini ya Sheria hii, kama mtu huyo-

- (a) amekiuka masharti ya kanuni za maadili;
- (b) hana uwezo wa kiutendaji;
- (c) amehukumiwa kufanya kosa linalohusiana na taaluma ya udaktari, udaktari wa meno na utaalum wa afya shirikishi;
- (d) ametiwa hatiani kwa kosa linalohusiana na utoaji huduma ya udaktari, daktari wa meno na mtaalam wa afya shirikishi; na
- (e) ana tatizo la kiakili na amethibitishwa hivyo na Bodi ya Madaktari Tanzania au mamlaka nyingine yoyote inayotoa leseni na kusimamia masuala ya afya katika nchi nyingine.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (2), maneno “kukosa sifa kutoa huduma” litatafsiriwa likijumuisha-

- (a) ukiukwaji wa masharti ya Sheria hii au kanuni;
- (b) kushindwa kuzingatia vigezo na masharti au mipaka ya usajili, uorodheshwaji au uandikishwaji kama daktari au daktari wa meno aliyesajiliwa, au mtaalam wa afya shirikishi kama itakavyokuwa;
- (c) kuwa na mgongano wa maslahi unaoathiri wateja na watoa huduma ya udaktari, udaktari meno au wataalam wa afya shirikishi waliosajiliwa, kuorodheshwa au kuandikishwa;
- (d) kufanya kazi pasipo kusajiliwa, kuorodheshwa au kuandikishwa au bila kuwa na leseni ya kutoa huduma;
- (e) kujaribu kutumia nambari ya cheti au mhuri wa daktari, daktari meno au mtaalam wa afya shirikishi mwingine aliyesajiliwa kama wa kwake au kujifanya daktari, daktari wa meno au mtaalam wa afya shirikishi aliyesajiliwa, kuorodheshwa au kuandikishwa;
- (f) kusaidia au kumwezesha isivyo halali mtu yeyote kutoa huduma kama daktari, daktari wa meno au mtaalam wa afya shirikishi;
- (g) kutoa taarifa au nyaraka za uongo kwa Baraza ili kupata cheti cha usajili, kuorodheshwa au kuandikishwa;
- (h) kujifanya ni daktari, daktari wa meno au mtaalam wa afya shirikishi aliyesajiliwa, kuorodheshwa au kusajiliwa au mwenye cheti cha usajili wa muda;
- (i) kumnyanyasa mteja kwa maneno, kimwili, kingono, kihisia au kwa namna nyingine yoyote;

- (j) kumshawisha mteja kubadilisha matakwa yake katika kuhusu maelekezo ya uangalizi wa afya;
- (k) kuacha kumpa huduma mteja anayehitaji huduma;
- (l) kutumia isivyo halali madawa au vifaa vingine vya mteja au mwajiri;
- (m) kushindwa kutoa taarifa za daktari, daktari wa meno au mtaalam wa afya shirikishi asiye na uwezo, mzembe au anayekiuka maadili ya kitaaluma na kuhatarisha afya ya mteja;
- (n) kushindwa kutumia busara katika kutoa taarifa za siri za mgonjwa; na
- (o) mwenendo mwingine wowote kama Baraza litakavyoona inafaa.

(4) Malalamiko yoyote chini ya kifungu hiki yataambatana na maelezo ya maandishi yatakayowasilishwa na mlalamikaji au mtu mwingine yeyote anayelalamika kwa niaba yake au mtu mwingine yeyote mwenye maslahi na kitendo kinacholalamikiwa.

(5) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (4), Baraza linaweza, kwa utashi wake, kuanzisha uchunguzi wa awali dhidi ya daktari, daktari wa meno au mtaalam wa afya shirikishi kama limejiridhisha kuwa taarifa lilizopokea na Baraza zinapelekea kufanyika kwa uchunguzi wa awali.

(6) Isipokuwa kwa malalamiko chini ya kifungu kidogo cha (1), hakuna uchunguzi wowote utakaoendelea isipokuwa pale mlalamikaji atakapowasilisha maelezo yake chini ya kiapo cha kisheria.

(7) Malalamiko yoyote yatakayowasilishwa kwenye Baraza yatakuwa kama yatakavyoainishwa kwenye kanuni.

Utaratibu wa uchunguzi

44.-(1) Baraza, pale litakapokuwa na maoni kuwa kuna kesi ya kujibu imeanzishwa na mlalamikaji, litaelekeza uchunguzi kufanyika.

(2) Baraza litatoa fursa kwa daktari, daktari wa meno au mtaalam wa afya shirikishi anayetuhumiwa kukiuka maadili, kufika mbele ya Baraza na anaweza kuwakilishwa mtu yeyote.

(3) Endapo daktari, daktari wa meno au mtaalam wa afya shirikishi atashindwa kufika kwenye uchunguzi wa shauri, bila sababu za msingi na Baraza limejiridhisha kuwa alipata taarifa, Baraza litaendelea na uchunguzi wa shauri dhidi ya daktari, daktari wa meno au mtaalam wa afya shirikishi kama vile mtaalam huyo alikuwepo.

(4) Baraza linaweza, baada ya kukamilika kwa uchunguzi uliotokana na masharti ya sheria hii:

- (a) kuagiza kuondolewa jina la daktari, daktari wa meno au mtaalam wa afya shirikishi katika daftari wa usajili, orodha au listi;
- (b) kuagiza daktari, daktari wa meno au mtaalam wa afya shirikishi kusita kwa muda kutoa huduma katika kipindi ambacho Baraza litaona kinafaa;
- (c) kuonya, kukaripia au kutoa onyo kali kwa daktari, daktari wa

meno au mtaalam wa afya shirikishi; au

(d) kuagiza mtaalam kulipa gharama za kuendesha uchunguzi au gharama nyingine zozote kama itakayoona inafaa.

(5) Msajili, ndani ya siku saba baada ya uamuzi wa uchunguzi, atawataarifu wahusika juu ya uamuzi wa Baraza.

(6) Baraza litakuwa na mamlaka ya kumwita shahidi yeyote na linaweza kumtaka shahidi huyo kuwasilisha nyaraka zozote kwa ajili ya uchunguzi.

Taarifa na uchapishaji wa maamuzi ya Baraza

45. Msajili, kwa kadri inavyowezekana na baada ya Baraza kukamilisha uchunguzi, atatoa taarifa ya uamuzi wa Baraza kwa Daktari, daktari wa meno au mtaalam wa afya shirikishi kuhusu shauri lililokuwa linamkabili.

Rufaa dhidi ya uamuzi wa Baraza

46. Mtu ambaye hajaridhika na uamuzi wa Baraza, ndani ya siku thelethini toka siku ya uamuzi, anaweza kuwasilisha maombi kwa ajili ya kupata uamuzi wa Mahakama kuu.

SEHEMU YA SITA MASHARTI YA FEDHA

Vyanzo vya fedha

47.-(1) Vyanzo vya fedha vya Baraza vitajumuisha-

(a) fedha zilizoidhinishwa na Bunge;

(b) fedha zozote au rasilimali ambazo zinaweza kuwa zimebainishwa au kukusanywa kutoka vyanzo vingine;

(c) mikopo iliyotolewa na Serikali au na mtu au chombo kingine chochote;

(d) ada na tozo nyingine zinazokusanywa kutokana na huduma zitolewazo chini ya Sheria hii;

(e) zawadi, misaada na michango;

(f) mapato yatokanayo na mauzo ya mali au vyanzo vingine vya mapato vinavyotambulika na Baraza; na

(g) fedha nyingine zozote zilizopokelewa, kupokelewa au zipo tayari kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Baraza.

(2) Ada na tozo zitaainishwa kwenye kanuni.

Taarifa za mwaka na mahesabu

48.-(1) Baraza kila mwisho wa mwaka wa fedha litaandaa taarifa ya utekelezaji ya mwaka ya shughuli zilizofanyika katika mwaka wa fedha na kuwasilisha taarifa hiyo kwa Waziri.

(2) Baraza litahakikisha taarifa ya fedha ya mwaka imeandaliwa na na kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya mwisho wa mwaka wa fedha.

(3) Taarifa za fedha zitajumuisha-

(a) taarifa ya utekelezaji wa kifedha;

(b) taarifa ya hali ya fedha;

(c) taarifa ya mtiririko wa mapato na matumizi;

- (d) taarifa ya mabadiliko ya faida au hasara; na
- (e) maelezo ya ufafanuzi wa taarifa za fedha;
- (4) Matumizi yote yatakuwa kama yalivyoidhinishwa na Baraza kulingana na makadiri yaliyoidhinishwa kwa mwaka huo wa fedha.

Uwasilishwaji wa taarifa ya fedha ya mwaka

49.-(1) Baraza litawasilisha kwa Waziri taarifa ya utekelezaji majukumu yake kwa mwaka husika ndani ya miezi sita baada ya mwisho wa mwaka wa fedha na taarifa hiyo itaambatana na:

- (a) nakala ya mahesabu yaliyokaguliwa,
 - (b) nakala ya taarifa ya Mkaguzi wa hesabu; na
 - (c) taarifa nyingine yoyote kama itakavyoagizwa na Waziri.
- (2) Mapema kadri itakavyowezekana, Waziri atawasilisha Bungeni taarifa ya ukaguzi wa mahesabu na taarifa ya mwaka ya Baraza.

Usimamizi na udhibiti wa fedha

50.-(1) Baraza litatunza vitabu vya hesabu na kuweka kumbukumbu sahihi za uendeshaji kwa mujibu wa viwango vya hesabu vya kitaifa.

(2) Baraza litawezesha upatikanaji na utunzwaji wa vitabu sahihi vya hesabu na kumbukumbu zinazohusu-

- (a) mali na madeni;
- (b) stakabadhi za matumizi ya fedha na matumizi mengineyo; na
- (c) taarifa ya hali ya fedha pamoja na taarifa inayoonyesha kiundani hali ya utendaji wa fedha itakayoandaliwa kila mwaka wa fedha.

(3) Fedha na rasilimali za Baraza zitatumika kulingana madhumuni ya Sheria hii.

(4) Matumizi ya fedha za Baraza yanatakiwa kufuatiliwa na kupitiwa.

Bajeti ya mwaka na bajeti ya nyongeza

51.-(1) Katika kipindi kisichozidi mwezi mmoja, kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha, Baraza, litaidhinisha bajeti kwa kiasi cha fedha kinachotarajiwa kupokelewa na kutolewa katika mwaka huo wa fedha.

(2) Iwapo katika mwaka wowote wa fedha, Baraza linahitaji kugawa fedha ambayo haikutengwa au kiasi ambacho ni zaidi ya kiasi kilichotengwa kwenye bajeti ya mwaka huo, Baraza litaidhinisha bajeti ya nyongeza itakayoonesha mgawanyo huo.

(3) Bajeti ya mwaka na bajeti ya nyongeza zitakuwa kwa namna itakavyoainishwa na kuelekezwa na Waziri.

Misingi ya uendeshaji

52.-(1) Baraza-

- (a) litafungua na kuendesha vitabu vyote vya fedha, leja, jarida na vitabu vingine vya ziada vya fedha kulingana na miongozo ya kijasibu; na
- (b) litapitia na kubadili nyaraka ili kuwezesha utunzaji sahihi vitabu vya hesabu za kifedha kadiri itakavyoelekezwa na mamlaka husika.

(2) Fedha zote zitakazopokelewa zitawekwa katika akaunti ya mapato na malipo yatafanyika katika akaunti ya matumizi.

(3) Hakuna matumizi yatakayotoka katika fedha za Baraza isipokuwa kama matumizi hayo ni sehemu ya mpango wa matumizi yaliyoidhinishwa na Waziri.

Mamlaka ya kuwekeza

53. Baraza linaweza, baada ya kupata idhini ya Waziri na kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kuwekeza kiasi chochote cha fedha kwa namna ambayo itaona inafaa.

SEHEMU YA SABA MAKOSA NA ADHABU

Makosa ya kutoa huduma kinyume cha sheria

54.-(1) Mtu yeyote kwa makusudi na udanganyifu anatoa huduma kama daktari, daktari wa meno au mtaalam wa afya shirikishi, huku akijua kuwa hana sifa za kutoa huduma hiyo, anafanya kosa na akipatikana na hatia, ataadhibiwa kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano lakini kisichozidi milioni kumi au kutumikia kifungo kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

(2) Mtu anayetoa huduma kama daktari, daktari wa meno au mtaalam wa afya shirikishi bila kusajiliwa, kuorodheshwa au kuandikishwa chini ya Sheria hii anafanya kosa, na akipatikana na hatia, ataadhibiwa kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mbili lakini isiyozidi milioni tano au kutumikia kifungo kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

(3) Mtu anayetoa huduma kama daktari, daktari wa meno au mtaalam wa afya shirikishi au anayepokea malipo bila kuwa na leseni halali ya kutoa huduma, anafanya kosa, na akipatikana na hatia, atatatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi milioni mbili au kifungo kisichopungua miezi mitatu lakini kisichozidi miezi mitano au vyote kwa pamoja.

Sura ya 219

(4) Kwa nyongeza ya adhabu zilizotolewa katika kifungo hiki, mahakama au Baraza, linaweza kuagiza dawa, sumu, sindano, vifaa vya upasuaji, vifaa vya udaktari au udaktari wa meno vinavyotumiwa au kumilikiwa na mtu aliyepatikana na hatia, kushughulikiwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Chakula, Dawa na Vipodozi.

Kosa la kusajiliwa kinyume cha Sheria

55. Mtu yeyote ambaye-

(a) anasaidia, anapata au kujaribu kupata usajili, uorodheshwaji au uandikishwaji au leseni ya kutoa huduma kwa;

(i) kutoa au kuwezesha kutoa maelezo ya uongo;

(ii) kutoa nyaraka za uongo au udanganyifu;

(b) anapokea fedha yoyote kutokana na kutoa huduma ya udaktari au udaktari wa meno, bila kusajiliwa, kuorodheshwa au kuandikishwa,

anafanya kosa, na endapo atapatikana na hatia, ataadhibiwa kulipa

faini isiyopungua shilingi milioni tano lakini isiyozidi shilingi milioni kumi au kutumikia kifungo kisichopungua mwaka mmoja au kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Adhabu za jumla
kwa baadhi ya
makosa

56. Mtu yeyote ambaye ameitwa na Baraza na:

(a) kushindwa kufika mbele ya Baraza bila sababu zozote za msingi; au

(b) anayeshindwa kutoa waraka wowote anaotakiwa kutoa, anafanya kosa, na akipatikana na hatia, leseni yake ya kutoa huduma itafungiwa au kufutwa na Baraza.

Adhabu kwa kutoa
utambulisho wa
uongo au kutoa
huduma kwa
kutumia leseni ya
kughushi

57. Mtu yeyote ambaye, kwa makusudi anaruhusu au kutumia kwa udanganyifu, jina, cheo au taarifa yoyote inayowakilisha sifa ya kutoa huduma ya udaktari au kupata malipo kama daktari, daktari wa meno au mtaalam wa afya shirikishi; anafanya kosa, na akipatakana na hatia, atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano lakini isiyozidi milioni kumi au kutumikia kifungo kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Adhabu kwa kuajiri
mtu asiye na leseni
halali

58. Mtu anayemwajiri mtu yeyote kutoa huduma kama daktari, daktari wa meno au mtaalam wa afya shirikishi kwa hadhi ya daktari, daktari wa meno au mtaalam wa afya shirikishi aliyesajiliwa, kuandikishwa au kuorodheshwa, bila kuwa na na usajili na leseni halali ya kutoa huduma hiyo, anafanya kosa, na akipatikana na hatia, atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano lakini isiyozidi milioni kumi au kifungo kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

SEHEMU YA NANE MASHARTI YA JUMLA

Kufuata Kanuni za
Maadili

59.-(1) Kutakuwepo na Kanuni za Maadili za taaluma ya Madaktari madaktari wa Meno na wataalam wa afya shirikishi ambayo itajulikana kama “Kanuni za Maadili”.

(2) Madaktari, madaktari wa Meno na wataalam wa afya shirikishi waliosajiliwa, kuandikishwa au kuorodheshwa chini ya sheria hii watatakiwa kufuata Kanuni za Maadili na ukiukwaji wowote wa masharti ya sheria hii kutapelekea “ukiukwaji wa maadili”.

Sifa za ziada

60. Mtu yeyote mwenye sifa za ziada ya alizosajiliwa, kuandikishwa au kuorodheshwa chini ya Sheria, anaweza kutuma maombi kwenye Baraza ili kutambua sifa hizo kwa namna itakavyoainishwa kwenye kanuni.

Mabadiliko ya
anwani

61. Kila daktari, daktari wa meno au mtaalam wa afya shirikishi, atamtaarifu Msajili mara moja mabadiliko yoyote ya anwani yake.

Kubakizwa kwenye Rejista, Orodha au Listi

62.-(1) Kila daktari, daktari wa meno aliyesajiliwa au mtaalam wa afya shirikishi aliyeorodheshwa au kuandikishwa na hafanyi shughuli za udaktari au utaalum wa afya atatakiwa kuendelea kuweka jina lake katika Rejista, Orodha na Listi kama itakavyokuwa kupitia uhuishaji wa kila mwaka.

(2) Maombi ya kuhuisha kuendelea kubaki kwenye daftari la usajili, orodha au listi chini ya sheria hii, yatawasilishwa kwenye Baraza kwa utaratibu maalum kabla ya cheti kilichopo kuisha muda wake na yataambatana na ada ya kuhuisha usajili.

(3) Endapo daktari, daktari wa meno au mtaalam wa afya shirikishi atashindwa kuhuisha kuendelea kubaki kwenye daftari la usajili, orodha au listi kabla ya cheti cha usajili, kuandikishwa, au kuorodheshwa, kuisha muda wake, Baraza linaweza kuhuisha usajili huo iwapo maombi yatatumumwa ndani ya miezi sita baada ya muda wa usajili kuisha.

(4) Iwapo muda wa miezi utapita bila daktari, daktari wa meno au mtaalam wa afya shirikishi aliyesajiliwa, ameshindwa kuhuisha usajili wake Baraza litasitisha kwa muda usajili kwa muda wa mwaka mmoja na iwapo daktari, daktari wa meno au mtaalam wa afya shirikishi baada ya mwaka mmoja kupita atashindwa kuhuisha usajili, Baraza litamfutia na kuondoa jina lake kwenye daftari la usajili.

Utambuzi wa makubaliano ya pamoja

63. Kutakuwa na utambuzi wa makubaliano ya pamoja wa watu waliosajiliwa kama madaktari, madaktari wa meno au wataalam wa afya shirikishi baada ya kuingia makubaliano ya utambuzi wa pamoja kati ya Baraza na mamlaka nyingine za taaluma.

Maombi ya marejeo

64.-(1) Mtu yeyote ambaye hataridhika na uamuzi wa Msajili kuhusu kusajiliwa, au kuandikishwa, kuorodheshwa anaweza, ndani ya siku thelathini toka siku ya kupokea uamuzi, kuliomba Baraza kufanya marejeo ya uamuzi huo.

(2) Baraza linaweza, baada ya kumsikiliza msajili na mtaalam, kutoa maelekezo kwa Msajili kadiri litakavyoona inafaa.

(3) Baraza linaweza kutengeneza kanuni kwa ajili ya kusimamia namna ya kusikiliza maombi ya marejeo.

Uchapishaji wa wataalam waliosajiliwa, kuandikishwa au kuorodheshwa

65. Msajili kabla ya tarehe 31 Machi kila mwaka au wakati mwingine wowote kama utakavyoelekezwa na Baraza, atatangaza majina ya watu waliosajiliwa, kuandikishwa au kuorodheshwa chini ya Sheria hii katika Gazeti la Serikali au chombo kingine cha habari.

Mamlaka ya kutengeneza Kanuni

66.-(1) Waziri, anaweza baada ya kushauriana na Baraza kutengeneza Kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa masharti chini ya sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (1) Kanuni zitaainisha:

(a) sifa, ambazo zitakazotambuliwa ili kumwezesha mmiliki wake

kusajiliwa, kuandikishwa, kuorodheshwa na kupata leseni, chini ya sheria:

- (b) kuweka viwango vya utendaji wa kitaalam kwa madaktari, madaktari wa meno na wataalam wa afya shirikishi;
- (c) kuweka viwango vya miongozo kwa ajili ya ukaguzi na kuidhinisha vituo vya mafunzo kwa vitendo;
- (d) fomu mbalimbali zitakazotumika chini ya Sheria hii;
- (e) programu ya uendeshaji wa mafunzo kwa vitendo;
- (f) utaratibu wa kuhuisha kubaki kenye daftari la usaji na leseni za kutoa huduma;
- (g) masuala ya rufaa chini ya Sheria hii;
- (h) masuala yanayohusu ada na kiasi kinachotakiwa kulipwa chini sheria hii;
- (i) kitu chochote ambacho, kwa maoni ya Baraza, ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa kazi na mamlaka ya Baraza chini ya Sheria hii.

Kufutwa kwa Sheria
Sura ya 152

67.-(1) Sheria ya Madaktari na Madaktari wa Meno imefutwa.

(2) Bila ya kujali Sheria iliyofutwa chini ya kifungu kidogo cha (1) kitu chochote au kitendo kilichofanywa au kilichotaka kufanywa chini ya sheria iliyofutwa, hakiko kinyume na masharti ya sheria hii, itachukuliwa kuwa kimefanywa au kuchukuliwa chini ya masharti ya sheria hii.

(3) Sheria zote ndogo zilizofanywa au kutolewa chini ya sheria iliyofutwa ambayo zilitumika baada ya kuanzishwa kwa sheria hii, zitachukuliwa kutungwa chini ya masharti ya sheria hii na zitaendelea kutumika mpaka pale zitakapofutwa na sheria ndogo zilizotengenezwa chini ya sheria hii.

JEDWALI

(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 5(5))

MASHARTI KUHUSIANA NA BARAZA

Uteuzi wa
mwenyekiti
msaidizi

1. Wajumbe watachagua miongoni mwa wajumbe kuwa Mwenyekiti Msaidizi wa Baraza na mjumbe huyo aliyechaguliwa atakaa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu.

Kipindi cha
kukaa
madarakani

2.-(1) Mjumbe, isipokuwa kama mamlaka ya uchunguzi imetengua uteuzi wake, au kuacha kwa namna yoyote ile kuwa mjumbe, atakaa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu lakini anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.

(2) Mjumbe aliyeteuliwa kwa mujibu wa ofisi yake ataacha kuwa mjumbe baada ya kuacha kuwa madarakani kwa mujibu wa ofisi iliyomteua kwenye Baraza.

Vikao vya Baraza

3.-(1) Baraza litakutana kwa muda na wakati utakaona unafaa kwa ajili ya kufanya shughuli zake, lakini litakutana angalau mara moja kila baada

- ya miezi mitatu.
- (2) Mwenyekiti, kama hatakuwepo, Mwenyekiti Msaidizi, anaweza muda wowote kuitisha mkutano maalum wa Baraza baada ya kuombwa na wajumbe wengi.
- (3) Mwenyekiti ama kwa kama hatakuwepo Mwenyekiti Msaidizi, ataongoza katika kila kikao cha Baraza na kama wote hawapo Mwenyekiti na Mwenyekiti Msaidizi, wajumbe waliopo watachagua mjumbe kutoka miongoni mwao kuongoza kikao.
- (4) Mjumbe wa Baraza aliyeshindwa kuhudhuria vikao viwili mfululuzi kwa mwaka bila ya kutoa sababu yoyote ataacha kuwa mjumbe na nafasi iliyoacha itajazwa.
- Akidi **4.** Akidi katika kila kikao cha Baraza kitakuwa ni mbili ya tatu ya wajumbe.
- Maamuzi ya Baraza **5.** Masuala yanayopendekezwa katika kikao cha Baraza yataamuliwa na kura nyingi za wajumbe waliopo na waliopiga kura, na inapotokea kura zinalingana, mtu anayeongeza katika kikao atakuwa na kura ya turufu ikiwa ni nyongeza ya kura yake ya maamuzi aliyopiga.
- Taarifa za kikao **6.** Msajili ataweka na kutunza taarifa za shughuli zote zinazofanywa au kuendesha katika kikao na taarifa ya kila kikao cha Baraza zitasomwa na kukubalika au kurekebisha na kuthibitishwa katika kikao kinachofuata cha Baraza na kusainiwa na mtu atakayeongoza kikao na Katibu.
- Kutokuhudhuria hakutahalalisha shughuli **7.** Uhalali wa kitu chochote au shughuli yoyote ya Baraza hazitaathiriwa na kutokuwepo kwa wajumbe wowote au kwa kosa lolote la uteuzi wa yeyote kati yao.
- Baraza litaendesha shughuli zake **8.** Baraza litaendesha shughuli zake lenyewe.
- Amri na nyaraka **9.** Amri zote, maelezo, au nyaraka nyingine zilizotolewa kwa niaba ya Baraza zitasainiwa na:
(a) Mwenyekiti; au
(b) msajili wa Baaraza aliyeidhinishwa kwa maandishi kwa niaba ya Baraza.
- Mhuri wa Baraza **10.**-(1) Baraza litakuwa na mhuri utakaowekwa na kutunzwa chini ya uangalizi wa Msajili.
(2) Kuwekaji wa mhuri wa Baraza kwenye nyaraka yoyote utathibitishwa na saini ya Mwenyekiti au Msajili.
(3) Nyaraka yoyote itakayodaiwa kutolewa na Baraza na kuthibitishwa kwa namna iliyotolewa chini ya aya ndogo (2) itachukuliwa kuwa ni hati halali.

Dar es Salaam,
13 Oktoba, 2016

UMMY A. MWALIMU
*Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii,
Jinsia, Wazee na Watoto*